OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

SHULE YA SEKONDARI ISANGAWANA

S.L.P 165

CHUNYA

05.12.2020

Kumb.Na.ISS/ST/JNI/13/.....

Mpendwa Mwanafunzi .....

S.L.P .....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ISANGAWANA WILAYA YA CHUNYA MKOA WA MBEYA -2021

1. **UTANGULIZI**

   Ninayo furaha kubwa kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.Shule ya sekondari Isangawana inapatikana kilometa 116 kutoka makao makuu ya wilaya ya Chunya na umbali wa meta 50 kutoka barabara kuu ya Tabora Chunya.Ukitoka stendi ya basi ya Isangawana iliyopo umbali wa meta 600 kutoka barabara kuu ya kwenda Chunya.

   Mhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe 11/01/2021.Aidha mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 zingatia kuwa wakati wote kigezo cha upimaji maendeleo yako ni NIDHAMU, TAALUMA NA KAZI ZA NJE Ukiwa ndani na nje ya shule.

MAHITAJI YA LAZIMA

- **SARE ZA SHULE**

(A)WAVULANA

i. Suruali mbili (2) za rangi ya zambarau zenye mshono wa kawaida
ii. Suruali mbili (2) za rangi ya kijani jeshi mshono wa kawaida
iii. Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi
iv. Sweta moja (1) rangi ya zambarau na sweta (1) yenye rangi ya kijani jeshi
v. Viatu jozi mbili (2) vyeusi vya kufunga na kamba vyembe visigino vifupi
vi. Soksi jozi mbili zenye rangi nyeusi
vii. Tai ya rangi ya zambarau moja (1) kijani jeshi moja (1)
viii. Godoro dogo na mashuka mawili rangi ya pinki

(B)WASICHANA

i. Sketi mbili (2) za zambarau zenye marinda ya kawaida (inchi moja)
ii. Sketi mbili (2) za rangi ya kijani jeshi zenye marinda ya kawaida (inchi moja)
iii. Shati mbili (2) za rangi nyeupe zenye mikono mifupi
iv. Sweta moja (1) rangi ya zambarau na sweta (1) yenye rangi ya kijani jeshi
v. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili (2)
vi. Viatu jozi (2) vyeupe vyenye visigino vifupi
vii. Skafu rangi ya zambarau moja(1) na kijani jeshi moja (1)
viii. Godoro la kulalia na mashuka mawili (2)

(C)SARE ZA MICHEZO

Wavulana waje na nguo za michezo kama vile bukta ya rangi ya bluu, fulana ya rangi ya njano na raba za michezo
Wasichana waje na nguo za michezo kama vile bukta ya rangi ya bluu, fulana ya njano na raba za michezo

MAHITAJI YA DARASANI

Mwanafunzi aje na vitu vofuatavyo: - Madaftari yasiyopungua kumi na tano (15), kalamu ya wino na penseli
Mzazi atagharamia nauli ya kwenda na kurudi shuleni pamoja na matibabu ya mtoto wako. Wanafunzi wote waje na fedha ya mahitaji mengine ya kibinadamu kama vile sabuni mafuta ya kupakaa, mswaki na dawa ya meno n.k.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na. 25 ya mwaka 1978 aidha inazingatia:-

(A) KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la LAZIMA
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
iii. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (prepation/ prepo)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo zitakazokuwepo
v. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
vii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa wanafunzi wake katika shule hii
viii. Ni mwiko kubadili jina bila kibali cha Afisa Elimu Mkoa au hati maalumu ya Mahakama
ix. Usichanganye vazi la shule na mavazi ya shule wakati uwapo shuleni au nje ya shule

x. Mzazi/mlezi yeyote atakaye mwandikisha shule mtoto kwa njia ya udanganyifu ikibainika mtoto wako ataondolewa mara moja

xi. Ni marufuku kubadili dini bila kibali maalumu cha Maahakama, wazazi, walezi wako

xii. Hakikisha unaripoti shuleni kwa muda uliyopangwa kwani ukichelewa kuripoti baada ya siku kumi na nne (14) nasafi yako itachukuliwa na mwingine

xiii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

xiv. Hauruhusiwi kuvaa mavazi ya kihuni, kukata nywele kihuni, huruhusiwi kufuga ndevu au kuvaa kofia au kuvaa suruali chini ya makalio (wavulana)

xv. Huruhusiwi kufuga kucha, kupaka rangi kucha, au kusuka nywele, kuvaa sketi fupi za kihuni wala kuweka dawa nywele (wasichana)

SHERIA ZA SHULE

TABIA NA MWENENDO (NIDHAMU)

i. Unatakiwa kuishi kwa amani,heshima na upendo.Sharti uwaheshimu walimu kama walezi wako na wanafunzi wenzako. Ni marufuku kupigana. Kutukana au kuanzisha/kushiriki vurugu za aina yeyote, kuchochea, kushiriki au kuanzisha mgomo ni kosa la jinai

ii. Lazima uthamini na kutunza mali ya umma hii ni pamoja na kutunza majengo ya shule ambayo nguvu za wananchi.Endapo utafanya uharibifu wa aina yoyote utarudishwa nyumbani hadi mzazi/mlezi wako atakapofidia gharama husika

iii. Ni mwiko kutoroka shule

iv. Ukipatikana na kosa la wizi, ulevi, uasherati, kuoa au kuolewa, kubaka, kulawiti, kupata/kutoa mimba/kusababisha mimba, kudharau au kuchana bendera ya Taifa utafukuzwa shule mara moja

v. Huruhusiwi kutumia mazingira ya shule kwa shughuli za kisiasa

vi. Huruhusiwi kuingia katika vilabu vya pombe na majumba ya starehe (GUEST HOUSE)

vii. Ni lazima wakati wote kuonyesha nidhamu ya hali ya juu wakati unaongea na walimu wako bila kutumia lugha chafu, kubishana, kukebei, kuzomea au kuguna n.k

viii. Kugomea adhabu ni kosa linaloweza kusababisha kufukuzwa shule aidha ni marufuku kupeleka malalamiko yako moja kwa moja kwa mkuu wa shule au nje ya shule

ix. Fujo, kelele, kuzomea, kukaa chini wakati mwalimu au mkubwa yeyote aingiapo darasani ni utovu wa nidhamu. Aidha huruhusiwi kutoka darasani ovyo bila ruhusa ya mwalimu kiongozi wako wa darasa

x. Ni lazima usimame kutoa salamu pindi mwalimu wako au mkubwa yoyote anapopita mbele yako

xi. Unatakiwa kutii na kufuata ratiba ya shule na kila kazi unayotakiwa kufanya mfano:- kuhudhuria vipindi vyote vya masomo na shughuli zote za nje

xii. Lazima kuheshimu kengele pamoja na kuwahi sehemu unayotakiwa bila kuchelewa

xiii. Huruhusiwi kuongea na wageni wako wakati vipindi vya darasani vinaendelea au pasipo ruhusa maalumu

xiv. Ni marufuku kutembea au kuingia vyumba vya walimu au wafanyakazi wasio walimu bila ruhusa maalumu

xv. Lazima kuheshimu tarehe ya kufunga shule.Endapo utachelewa kufika shuleni hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako

xvi. Kila mzazi/Mlezi ahakikishe mtoto wake anahitimu elimu ya sekondari

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu mali ya umma kwa makusudi
8. Kudharau bendera ya taifa na wimbo wa taifa
9. Kuoa au uolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba (ndani na nje ya shule)
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea, kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
13. Kukataa adhabu kwa makusudi

MAMBO MENGINE

Pamoja na barua hii zingatia viambatanisho vifuatavyo:

1. Fomu ya uchaguzi wa afya ya mwanafunzi ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali na fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule utakaporipoti shuleni
2. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI ISANGAWANA

.....

TIPSON MLELWA GIDEON
MKUU WA SHULE
0744154630/0627576842/tipgideon07@gmail.com

HEADMASTER
SANGAWANA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 165
CHUNYA - REY

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

SHULE YA SEKONDARI ISANGAWANA

1. Mimi _____ Msichana/Mvulana nimekubali kuingia kidato cha kwanza (I) katika shule ya sekondari Isangawana kama mwanafunzi tarehe _____ Nitafika shuleni bila kuchelewa.
2. Nitatii sheria za shule, sitajihusisha wala kuchochea migomo shuleni. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea
3. Sahihi ya mwanafunzi _____ Tarehe _____

SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI:

1. Mimi _____ nimekubali mtoto wangu _____ asome katika shule ya sekondari Isangawana kuanzia tarehe _____
2. Ninaahidi kumpa vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua
3. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea
4. Ninakubali mtoto wangu amekubaliwa kuingiwa katika shule ya sekondari Isangawana
   Kama mwanafunzi wa kutwa na ataendelea hivyo hadi atakapomaliza kidato cha IV. Naelewa nafasi katika shule za bweni ni haba sana, hivyo mimi wala mwanangu hatutamsumbua mkuu wa shule kwa vyovyote kuhusu mipango ya malazi au uhamisho kwenda shule za bweni
5. Anwani yangu ya kudumu ni:-
   .....
   .....
   .....
6. Namba ya simu: .....
7. Sahihi .....
8. Tarehe .....

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION OFFICE

CHUNYA DISTRICT COUNCIL

ISANGAWANA SEKONDARY SCHOOL

P.O.BOX 165,

CHUNYA

DATE .....

TO MEDICAL OFFICER

.....

.....

PART A:

MR/MISS: .....

Please examine the above named pupil to his/her Physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following:

1. Hemoglobin .....
2. P.V.Bleeding .....
3. Sight .....
4. Blood pressure .....
5. Urine for sugar and pregnant test .....
6. Stool for routine examination .....
7. Asthma .....
8. Skin diseases .....
9. Leprosy .....
10. Any deformity.....
11. Epilepsy.....
12. Pulmonary tuberculosis .....
13. Neurosis .....
14. General diseases .....

PART B;

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named pupil and consider that she /he is physically fit and mental fit to join the school

.....

Signature (Dr)